JAMHURI YA KENYA

Wizara ya Mipango na Maendeleo ya Nchi

# Mfumo Shirikishi wa Kitaifa wa Uchunguzi na Utathmini

# NIMES

Tunakuza na kuboresha maendeleo



## Swali: Mfumo wa NIMES ni nini?

Jibu: NIMES ni ufupisho wa Mfumo Shirikishi wa Kitaifa wa Uchunguzi na Utathmini katika Kiingereza. Ni chombo maalum cha sera kilichobuniwa 2004 ili kuchunguza maendeleo yaliyopatikana kwenye 'Mbinu za Kufufua Uchumi' (ERS), na ambacho kwa sasa kimeimarishwa ili kuwezesha kutolewa kwa ripoti za matokeo ya sera na maendeleo, ikiwa ni pamoja na 'Taswira ya Kenya ya 2030 (Kenya Vision 2030) na Malengo ya Maendeleo ya Milennia (Millennium Development Goals). NIMES ni chombo cha usimamizi chenye lengo la kuonyesha uwazi kwenye sera za matumizi ya pesa na utekelezaji wa mipango ya Serikali, Mashirika ya Kijamii, Mashirika ya Kibinafsi na washirika wa kimaendeleo. Mfumo huu pia unahusika na usimamizi wa mipango na miradi kwa kuchunguza, kutoa ripoti, kutathmini ukuzi na matokeo ya maendeleo na matumizi ya rasilmali.

## Swali: Je ni kwamba kuchunguza na kutathmini mipango na miradi ya maendeleo ni jambo jipya nchini Kenya?

Jibu: Jambo hili limekuwa likifanyika nchini Kenya, hasa kwenye miradi. Mnamo mwaka wa 1983, mfumo wa kuchunguza na kutathmini mipango ulipendekezwa kwenye Mpango wa Kutekeleza Maendeleo Mashinani Kupitia Mipango Wilayani (District Focus for Rural Development Strategy DFRDS). Tukilinganisha mkakati wa DFRDS na NIMES, tutagundua kwamba NIMES inaangazia

mengi zaidi, hasa kwa kuwa inalenga Maendelo ya Kitaifa na pia mashinani. Mbali na kuangazia na kuchuguza miradi, NIMES pia inashughulika kuchunguza na kutathmini sera na mipango, ikiwa ni pamoja na Mipango ya Marekebisho Serikalini ambayo italeta maendeleo na kuimarisha maisha ya jamii.

## Swali: Je NIMES itatekelezwa vipi?

Jibu: NIMES inalenga sehemu tano ambazo shughuli zake za uchunguzi na utathmini zitazingatiwa. Sehemu zenyewe ni;

- Ukusanyaji wa habari zinazoweza kupimwa (quantitative data) au zile zinazotokana na hali au maoni (qualitative data), kuhifadhiwa kwa habari hizo na kuundwa kwa viashirio vinavyoweza kueleza au kudokeza jawabu.
- Uchambuzi wa utafiti na matokeo yaliyopo.
- Usambazaji wa jinsi ya kuelimisha na kuwepo kwa utambuzi wa hali ilivyo.
- Uchunguzi na utathmini wa miradi.
- Ukuzaji wa ujuzi wa utendakazi na upatanishi wa Sera za Serikali.

## Swali: Ni nini hasa kitajumuishwa katika mipango au mikakati hii mitano ya NIMES?

Jibu: (i) Ukusanyaji wa habari (data) zinazoweza kupimwa au zile zinazotokana na hali au maoni, kuhifadhiwa kwa habari hizo na kuundwa kwa viashirio vinavyoweza kueleza (kudokeza) jawabu. Nia hapa ni kutambua Viashirio ambavyo vitasaidia juhudi za kuchunguza sera

zinazotekelezwa na hata mipango inayotekelezwa nyanjani na kitaifa, kama vile, Taswira ya Kenya ya Mwaka wa 2030 (Kenya Vision 2030) na Mbinu za Ufufua Uchumi (ERS), na zile za kimataifa kama vile Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs). Juhudi za kutumbua viashirio zitafanywa kupitia kwa wizara za serikali, Mashirika ya Kiserikali, Mipango ya Mabadiliko ya Kiserikali, na pia Mashirika ya Kijamii na Sekta ya Kibinafsi.

(ii) Uchambuzi wa Utafiti wa Matokeo yaliyopo: Sehemu hii ya NIMES inaangazia kubuni sera ambazo zitatoa habari kuhusu jinsi fedha za Serikali zitakavyotumiwa. Uchambuzi huu utatilia maanani matokeo ya utafiti yanayotokana na ukusanyaji habari na takwimu ya watu, kazi inayofanywa na Kituo cha Kenya cha Kuhifadhi Takwimu za Kitaifa (Kenya National Bureau of Statistics - KNBS), Ukadiriaji-Shirikishi wa Umaskini (Participatory Poverty Assessment) unaofanywa na Idara inayoshughulikia Mipango ya Sehemu mbali mbali za nchi (Sectoral Planning Directorate) ya Wizara ya Mipango na Maendeleo ya Nchi, na Idara zingine rasmi zilizopo.

(iii) Uenezaji wa jinsi ya kutoa mafunzo na kujenga hisia za watu. NIMES itasaidia kuleta maridhiano na uelewano juu ya sera za kitaifa na zile za kimataifa na kusisitiza umuhimu wa Kenya kuchunguza hatua iliyopiga kwa kutilia maanani sera hizo. Madhumuni hapa ni kusaidia kuendeleza na kukuza Uchunguzi na Utathmini wa Kimataifa na nyanjani kupitia mafunzo au uzoefu, na pia kuanzisha mafunzo ya kijamii yatakayowezesha wahusika kutoa maoni yao vilivyo, maoni kuhusu huduma wanazopata na manufaa ya utekelezaji mipango au miradi ya Serikali.

(iv) Kuchunguza na Kuthamini Miradi: Kuchunguza miradi ndio sehemu ya kuchunguza na kutathmini

inayojulikana sana nchini Kenya. Hata hivyo, bado kuna umuhimu wa kuwepo kwa kanuni za mipango, ukadiriaji, uchunguzi na utathmini wa miradi iliyogharamiwa na kutekelezwa na Serikali, Wahasirika wa Kimaendeleo, Mashirika ya Kijamii na Sekta ya Kibinafsi. Kuanzishwa kwa sheria zinazosimamia kanuni za uchunguzi kutaleta uwazi kwenye utekelezaji wa miradi midogo (miradi yenye gharama chini ya shilingi milioni moja) inayotekelezwa kwa kutumia pesa kutoka humu nchini, miradi mingine midogo (yenye gharama ya shilingi milioni moja hadi milioni tano) na miradi mikubwa (yenye gharama zaidi ya milioni tano).

(v) Ukuzaji ujuzi kazini na uratibishaji wa Sera. Ili NIMES ipate kufaulu, kuna haja ya kukuza ujuzi katika ngazi zote kama juhudi za kufanikisha Uchunguzi na Utathmini na kupeana mazingira mema ya kutekeleza Sera hii. Hivyo basi, ujuzi uliopo wa kuendeleza uchunguzi na utathmini wa kitaifa na hata mashinani katika Idara za Serikali, Mashirika ya Serikali na kwenye Mipango ya Merekebisho Serikalini utakadiriwa, mapengo yaliyopo yajulikane na Mipango ya mafunzo ianzishwe ili kuyajaza mapengo hayo. Mbali na hayo, Sera ya Kitaifa ya Kuchunguza na Kutathmini itaanzishwa ili kuhakikisha kupatikana kwa habari kuhusu uchunguzi na utathmini kwa njia laini kwenye mfumo huu.

## Swali: Ni nani atakayetekeleza Mfumo wa NIMES?

Jibu: Idara ya Uchunguzi na Utathmini (MED) iliyopo katika Wizara ya Mipango na Maendeleo ya Nchi ina Jukumu la Kitaifa la kuratibisha shughuli za NIMES. Pia kuna kamati ya usimamizi ya kitaalamu

(TOC) itakayoongoza mipango na mikakati ya NIMES, na Kamati Elekezi ya Kitaifa (NSC) itakosaidia Serikali kuweka pamoja rasilmali zinazohitajika. Vikundi vya Kitaalamu vya Ushauri (TAGs) vitano vitatoa miongozo ya kitalamu juu ya mikakati mitano inayolengwa. Wizara, Mashirika ya Kiserikali na Wilaya pia zinastahili kubuni kamati kama hizi ili kuziwezesha kutoa huduma kwa njia inayofaa.

## Swali: Jukumu la MED ni nini?

Jibu: MED ina jukumu la kutoa makala yafuatayo ya kila mwaka;

- Ripoti ya kila mwaka ya maendeleo (kuhusu Taswira ya Kenya ya 2030 (Kenya Vision 2030), na Mbinu za Kufufua Uchumi (Economic Recovery Strategy)
- Ripoti ya kila mwaka ya uchunguzi wa miradi
- Ripoti ya kila mwaka kutoka Wilayani ya uchunguzi na utathmini
- Ripoti ya uchambuzi wa matumizi ya pesa za Umma
- Habari zingine na shughuli zilizopo chini ya idara hii.

## Swali: Je NIMES itapataje habari za kuiwezesha kuandika ripoti yake ya uchunguzi?

Jibu: MED haitajishughulisha na kupokea habari za msingi, bali itatumia habari na ripoti zilizotayarishwa na wizara zingine, Mashirika ya Kiserikali, Mashirika ya Kijamii, Sekta ya Kibinafsi na Washirika wengine wa maendeleo. Itatumia

takwimu za idadi ya watu na takwimu zingine kutoka kituo cha Takwimu cha Kitaifa cha Kenya (KNBS) na takwimu za Ukadiriaji wa Umaskini unaofanywa na Idara inayoshughulikia Mipango ya Sekta mbali mbali za nchi (Sectoral Planning Directorate), iliyo chini ya Wizara ya Mipango na Maendeleo ya Nchi. MED pia itatumia takwimu za kazi kutoka Wizara zingine.

## Swali: Je, itakuwa lazima kwa idara zingine za Serikali za Mashirika ya Kiserikali, Mashirika ya Kijamii, Sekta ya Kibinafsi na Washirika wa Maendeleo kutoa ripoti zao kwa MED?

Jibu: La, haitakuwa lazima kwa idara hizi kutoa ripoti zao kwa MED bali Sera ya Kitaifa ya Uchunguzi na Utathmini itaanzishwa ili kuweka mazingira yatakayowezesha MED na washirika wake kubadilishana habari. Kutoa ripoti kwa MED kutafanywa kila baada ya kipindi kitachowekwa. Kwa hivyo hakutakuwa na usumbufu kwenye kazi za idara au mashirika mengine. Hatimaye, ripoti zote za uchunguzi zitapelekwa Bungeni na kwa Baraza la Mawaziri na kujumushwa kwenye mipango na Bajeti ya Nchi.

## Swali: Je MED ina jukumu lolote kwa umma?

Jibu: MED haina budi kuipa Umma maelezo kuhusu utekelezaji wa shughuli zake. Matokeo ya uchunguzi wake hayana budi kutafsiriwa katika lugha nyepesi, na ikiwezekana katika Lugha ya Kitaifa (Kiswahili). Mikutano ya kuelekezea sera pia itaandaliwa Wilayani na Mashinani. Mfumo wa uenezaji wa jinsi

ya kutoa mafunzo na kujenga hisia za watu utatumiwa pia kama njia ya kupitishia ripoti za Utaratibu wa Kuchunguza na Kukagua kwa Usawa Serikali za Kiafrika (APRM) hadi kwenye utaratibu wa Kitaifa wa Mipango na Uundaji Sera.

## Swali: Je kuna ujuzi wa kutosha wa kutekeleza NIMES?

Jibu: Kwa kuwa Kenya haijawa kwenye mstari wa mbele wa Uchunguzi na Utathmini, uwezo wake haujakuzwa vilivyo. Ukadiriaji wa uwezo wa nchi wa kuchunguza na kutathmini mipango na miradi utafanywa katika ofisi kuu za kitaifa na nyanjani na mipango ya mafunzo kuandaliwa kupitia kwa Taasisi ya Kenya ya Mafunzo ya Kitawala (KIA) na Vyuo Vikuu. Taasisi zingine za Kitaifa za Utafiti kama vile Taasisi ya Kenya ya Sera za Umma na Uchambuzi wa Utafiti (KIPPRA) pia zitakuwa muhimu katika hatua hii ya utekelezaji wa Mfumo wa NIMES, MED itaanda mkutano wa kila mwaka wa kuadhimisha wiki ya shughuli za Uchunguzaji na Utathmini ili kuendeleza uwezo utakaowezesha ukuzaji wa uchunguzi na Utathmini Nchini.

Kwa maelezo zaidi au maoni kuhusu Mfumo-Shirikishi wa Kitaifa wa Uchunguzi na Utathmini (NIMES, Wasiliana na:

Mkurugenzi, Idara ya Uchunguzi na Utathmini,
Wizara ya Mipango na Maendeleo ya Nchi,
Jumba la Mikutano la Kenyatta (KICC),
Orofa ya 24 S.L.P 47697-00100 Simu: 227411,
mkondo (Ext) 22199
Kipepesi: medmpdn@yahoo.com